**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu, lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa**

Nilifika katika stani ya magari ___1___ niliona watu wa kila aina. Wengine walikuwa ni wasafiri, wengine ni ___2___ wa kubeba mizigo na wengine walikuwa wanafunzi wa shule. Pia palikuwapo watalii ambao walikuwa bado hawajatosheka na ___3___ picha mbalimbali. Mara alitokea mzee mmoja ambaye hakujua sana habari za ___4___ stesheni. Naye aliuliza kuhusu kila kitu ___5___. Kwanza aliulizia mahali ambapo tikiti ___6___. Alipoonyeshwa, aliuliza gari ___7___ saa ngapi. Kila alipojibiwa swali hili, aliuliza lile.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ambako | ambayo | ambapo | ambamo |
| 2. | wachuuzi | makuli | mahamali | utingo |
| 3. | kupigisha | kupiga | kupigiwa | kupigana |
| 4. | hapa | humo | huko | pale |
| 5. | alichokiona | aliloona | aliona | aliyoona |
| 6. | hukatiwa | huuziwa | huchukuliwa | husambaa |
| 7. | limeondoka | lingeondoka | linaondoka | liliondoka |

Niliamka ___8___ vishindo ___9___ kugundua kwamba kila mtu alikuwa amejifunika ___10___ na wote wamelala fofofo. Sikuamini macho yangu ___11___ saa na kugundua nilikuwa nimechelewa. Kwanza nilikasirika kwa vile msichana wangu niliyeajiri kama ___12___ hakuwa ameamka ili kutayarisha chai. Siku hiyo nilitakiwa kwenda kwa mahojiano ya kazi ambayo ___13___ ukurasa mpya katika maisha yangu. Isitoshe niliamini kwamba Mungu alikuwa ameninyoshea mkono wa ___14___ kwa vile nafasi za kazi zilikuwa zimeadimika. Nilifanya ___15___ huku nikiomba Mungu.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 8. | na | vya | kwa | wa |
| 9. | baada ya | kabla ya | nyuma ya | mbele ya |
| 10. | kupukupu | chapuchapu | gubigubi | katakata |
| 11. | nilipochungulia | nilipochunguza | nilipochungua | nilipochukuliwa |
| 12. | kitwana | tasa | msusi | kijakazi |
| 13. | ingenifunga | ingenifungulia | ingenifungia | ingenifungua |
| 14. | baraka | birika | tahania | tanzia |
| 15. | hofu | kimasomaso | hima | kwa mkato |



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kuanzia swali nambari 16 -30, chagua jibu kulingana na maagizo***

16. Chagua sentensi ambayo si hali ya kutendwa.
A. Chakula kinapikwa na Roda.
B. Milango yote ilifungwa na Maria.
C. Nguo zetu zinafuliwa na dobi.
D. Juma amekunywa maziwa yote.

17. Tunasema pakacha la machungwa na baraza la _
A. mawaziri
B. chifu
C. vitabu
D. watu

18. Chagua sentensi yenye kwa ya umilikaji.
A. Alikunywa chai kwa bilauri.
B. Wao hutumia kuni kwa kupikia.
C. Ametoka kwa mwalimu mkuu.
D. Kuuliza kwangu kulinisaidia

19. Andika tarakimu hii kwa maneno. 10,000,001
A. Milioni kumi na moja.
B. Laki moja na moja.
C. Milioni moja kumi na moja.
D. Kumi milioni na moja.

20. Chagua sentensi yenye kielezi cha idadi.
A. Waliimba sana usiku huo.
B. Wameenda mara chache kulingana naye.
C. Ng'ombe watano walishambuliwa vibaya.
D. Waliingia mmoja mmoja ili watoshee.

21. Chagua sentensi iliyotumia kihusishi kwa njia ifaayo.
A. Huree! Mali yote yaliibwa usiku wa kuamkia leo.
B. Pole! Nyote mmenusurika kutoka kwenye ajali hiyo.
C. Alhamdulilahi! Amejifungua pacha wawili wa kiume.
D. Ebo! Furaha iliyoje kujishindia shilingi milioni moja.

22. Yapi si maana ya neno kata.
A. Kutokubali jambo kabisa.
B. Eneo la utawala.
C. Kifaa cha kuchotea maji.
D. Kutenganisha kitu kwa kifaa kama vile kisu.

23. Chagua methali yenye maana sawa na; Cha kuvunda hakina ubani.
A. Kulea mimba si kazi, kazi ni kulea mwana.
B. Mwenye macho haambiwi tazama.
C. Mstahimilivu hula mbivu.
D. Ajali haina kinga.

24. Chagua jina ambalo haliambatani na mengine.
A. Kichinjamimba
B. Mzuwanda
C. Mwanambee
D. Kifungamimba

25. Chagua sentensi yenye kivumishi cha pekee kisichoonyesha ubaguzi.
A. Kalamu yote imepakwa rangi.
B. Mwanafunzi yeyote atalipiwa karo.
C. Karamu nyingine itaandaliwa.
D. Mikeka mingi hununuliwa katika duka kuu.

26. Roda ni *mkia wa mbuzi*. Yaani ______
A. ni mjeuri
B. ni mkaidi
C. ni jasiri
D. ni ovyo

27. Andika kwa wingi. Kobe alilivamia shamba langu na kula kobwe.
A. Kobe waliyavamia mashamba yangu na kula kobwe.
B. Kobe waliyavamia mashamba yetu na kula makobwe.
C. Makobe waliyavamia mashamba yetu na kula makobwe.
D. Makobe waliyavamia mashamba yetu na kula kobwe.

28. Asubuhi moja nilipokuwa nikielekea shuleni, kivuli changu kilikuwa upande wa kulia. Je, shule ilikuwa upande gani?
A. Kusini
B. Kaskazini
C. Mashariki
D. Magharibi

29. Ni sentensi gani inayotumia taraa vizuri.
A. Nitamsaidia taraa atakuja.
B. Alipomwona simba alitoka taraa.
C. Nilimla ng'ombe mzima taraa kuku.
D. Nilienda shuleni taraa nilikuwa mgonjwa.

30. Chagua jibu linaloonyesha vipande vya mshororo.
A. Tarbia, Takhmisa
B. Ukwapi, utao
C. Mwandamizi, vina
D. Malenga, manju



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**_Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40_**

Kati ya sehemu zilizo muhimu sana katika mazingira ya binadamu ni misitu. Wataalamu wa masuala ya mazingira wanapendekeza angalau asilimia kumi ya ardhi ya kila nchi kuwa na misitu. Baadhi ya nchi zimefikia kiwango hiki na labda hata kukipiku ilhali nyingine ziko chini ya kiwango hiki. Hali hii hutokana na matumizi mabaya ya misitu yenyewe, ufywekaji wa miti ili kuchoma makaa, unyakuzi wa misitu na ufyekaji ili kuanzisha kilimo.

Ni wazi kuwa uhifadhi wa misitu una manufaa tumbi nzima kwa binadamu. Hata hivyo binadamu mwenyewe ndiye anayeiangamiza misitu yenyewe. Watu wenye mate ya fisi wamekata miti kiholela kwa ajili ya kupata kuni na kuchomea makaa ya kuuza. La kushangaza ni kuwa, watu hawa **_hawadiriki_** kupanda miti mingine kufidia ile waliyoikata. **_Wengine kwa kutojua wanajiletea maafa, hupanda miti ambayo inakausha vyanzo vya maji na kuchangia kuenea kwa kasi kwa jangwa_** . Hali kadhalika wapo warina asali ambao katika juhudi zao za kurina husababisha kuteketea kwa misitu.

Misitu husaidia kuhifadhi ardhi isimomonyolewe na kuondolewa na maji ya mvua kwa urahisi. Mmomonyoko wa ardhi husababisha maafa na madhara makubwa sana kwa watu. Aidha misitu husaidia kurekebisha mtiririko wa maji ya mito; kwa sababu misitu huifanya mito isifurike kupita kiasi. Sote tunajua madhara yanayoweza kusababishwa na gharika au mafuriko yanayotokana na kunyesha kwa mvua za mzo. Kuwapo kwa misitu pia huzuia kiwango cha takataka kama mchanga, ardhi au majani yanayochukuliwa na maji ya mito. Kwenye mabonde ya baadhi ya mito, huenda kukawa na miradi kadhaa mathalani ya kutengeneza nguvu za umeme au mashamba ya kumwagiliwa maji. Ikiwa takataka zote zibebwazo na maji hazitachunjwa, basi uwezekano wa kuharibiwa kwa miradi hii ni mkubwa.

Maendeleo ya utafiti wa kisayansi yameonyesha mchango mkubwa unaotokana na miti hasa ya kienyeji kuhusiana na dawa zinazotumiwa kuyatibia magonjwa sugu. Isitoshe, kuwepo kwa karatasi zinazotumiwa kuuelewa umuhimu wa misitu. Tusipowajibika basi kuna hatari ya **_maisha ya kesho_** kuwa magumu kwa sababu ya matatizo ya ukosefu wa maji, kuwepo kwa majangwa na kukosa malighafi za kimsingi ambazo ni nguzo za uchumi wetu wa leo.

Kifungu cha katiba kinachohusu mazingira na mali ya asili kinasisitiza suala la uhifadhi wa mazingira. Kila mwanajamii basi ana jukumu la kuilinda misitu na kuepuka mazoea ambayo yanaiangamiza la sivyo tutakuwa tunajichimbia kaburi.

**31.** Kulingana na kifungu,
A. Misitu ndiyo sehemu muhimu sana kuliko zote kwa binadamu
B. Pendekezo la wataalamu ni sehemu nyingine zote zichukue asilimia tisini huku inayobaki ikitengewa misitu
C. Hakuna taifa ambalo limefikia kiwango kinachotakikana kutengewa misitu
D. Ufyekaji wa miti huimarisha kilimo cha maskini

**32.** Ni jibu gani ambalo **_si sahihi_** kulingana na aya ya **_pili_**?
A. Ukataji wa miti unapaswa kuandamana na upandaji
B. Shughuli yenye faida yaweza kuishia kuleta hasara
C. Ukosefu wa maarifa unaweza kusababisha hasara
D. Jaribio la kupanda miti linastahili kuepuka panapotolewa maji

**33.** Ujumbe uliopigiwa kistari katika aya ya pili unaweza kufupishwa kwa methali gani?
A. Kajigeuza chachandu kujipalia makaa
B. Baada ya dhiki faraja
C. Ujanja wa nyani huishia jangwani
D. Jambo usilolijua ni kama usiku wa giza

**34.** Maana ya **_hawadiriki_** kulingana na kifungu ni:
A. hawawahi
B. hawaambulii
C. hawarauki
D. hawawazii

**35.** Tunaweza kusema kuwa, kulingana na aya ya kwanza
A. Miti hukatwa kutokana na tamaa ya mali
B. Miti hukatwa kutokana na upendo na uzalendo
C. Miti hukatwa kutokana na umaskini
D. Miti hukatwa kama njia ya kuhifadhi mazingira



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**36.** Mradi wa kutengeneza nguvu za umeme unaweza kuathiriwa na
- A. takataka zinazobebwa na maji bila kuchujwa
- B. mabonde ya baadhi ya mito
- C. mashamba ya kunyunyuziwa maji yaliyo karibu
- D. Maji mengi kupita kiasi

**37.** Chagua hasara za kutohifadhi misitu kwa mujibu wa kifungu
- A. maisha magumu, ukosefu wa maji, jangwa na ukosefu wa malighafi
- B. Kunyauka kwa majani, kupoteza urembo, kasi ya jangwa
- C. upepo mkali, jua kali, kunyauka kwa maua
- D. Kuporomoka kwa majengo, kupoteza mvuto, jangwa na upepo mkali

**38.** Maisha ya kesho ni sawa na
- A. maisha tuyaishiyo leo
- B. maisha yaliyopita
- C. maisha ya tabu
- D. mustakabali

**39.** Anwani ifaayo makala haya ni
- A. Umuhimu wa mazingira
- B. Maendeleo mashinani
- C. Umuhimu wa misitu
- D. Hasara za uharibifu wa mazingira

**40.** Kulingana na aya ya mwisho,
- A. mazingira huhifadhiwa kupitia kwa kifungu cha katiba
- B. Binadamu hujiletea majuto kwa kutoepuka mienendo isiyokubalika
- C. Mazingira huharibiwa na hulka zisizofaa za binadamu
- D. Mwanajamii anastahili kufuata mshawasha wa katiba

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50***

Hapo zama za mababu zetu aliishi jamaa mmoja ambaye chimbuko lake halikueleweka barabara na wakazi wa eneo hilo. Hivyo basi hakuna hata mtu mmoja aliyelijua jina lake asilia ila walimlakabu ndugu Mahewa kwa kuwa alipenda sana kutumia usafiri wa hewani kinyume na wenzake ambao hata viatu vya kutembelea ardhini hawakuwa navyo. Sifa zake zilizagaa kama moto nyikani msimu wa ukame. Nyumba yake ilisifika ghaya kutokana na wajihi na wasifu wake wa nje. Jumba lenyewe lilikuwa fahari kwa yeyote aliyelitupia jicho. Lilijengwa ka mawe adimu na kuezekwa kwa vigae vyekundu vilivyoliongezea haiba na kulifanya lizungumziwe kwa kirefu na kila mkazi. Wengi walidai kuwa ndugu Mahewa aliishi katika ikulu.

Sifa moja iliyomtenganisha ndugu Mahewa na wanakijiji wengine ni utajiri wake wa kupindukia. Ilisemekana kwamba alikuwa na safu ya biashara huko jijini kiasi cha watu kudai kuwa alikuwa mmiliki wa jiji lote na watu wake. Japo hili haliwezekani, ndugu Mahewa alikuwa mkwasi wa kutajika.

Naam, utajiri uingiapo, ukafiri hujongea. Kutokana na maendeleo ya kiuchumi, ndugu Mahewa aliibwaga tabia yake ya ucha Mungu. Kiburi nacho kikamvaa kama lubega. Watu walipotaka kujua kwa nini hakupenda kutangamana na watu alijibu "Aaa! Haya mambo ya akina baba kabwela siyawezi. Mimi ni mtu wa juu si mtu wa chini kama nyinyi. Uhitaji wa baadhi yenu unaweza kuambukiza." Alichosahau ndugu Mahewa ni kuwa aliyempa kiti ndiye aliyenipa kumbi.

Siku moja Mzee Busara alimwendea kumtaka usafiri wa gari. Asubuhi hiyo mjukuu wake wa pekee alishikwa na maradhi ya ghafla na Mzee Busara hakujua la kufanya ila kumwendea Mzee Mahewa. Mzee Busara alikuwa na bahati kwa kuwa ndugu Mahewa alikuwa nyumbani asubuhi hiyo. Hilo lilikuwa jambo tukizi na adimu. Alipofika alimsabahi na kumweleza matakwa yake kwa upole. Ndugu Mahewa alimsikiliza kwa muda kabla ya kumkatiza, "Ndugu mzee ............ unaitwa nani vile?" Aliuliza huku ameibirua midomo yake kama mtu anayetazama kinyaa.

"Jina langu ni Busara. Nilikuwa kwenye kundi moja la tohara na babako, " alisema Mzee Busara. Ndugu Mahewa alimwangalia kuanzia miguuni hadi utosini kisha akamwambia , " Sikiliza Mzee. Naona una hadithi nyingi sana zisizo na mashiko. Mimi nina safari muhimu sana kwenda ng'ambo. Sina muda wa kuyafanya hayo unayoyataka. Toka sasa!"

Mzee Busara alishika tariki kurudi zake nyumbani huku uchungu na huzuni nyingi vikimtafuna moyoni. Alimlaani ndugu Mahewa kimoyomoyo, " mtu hana huruma ya kibinadamu. Muhimu kwake ni hizo safari zake za Ng'ambo. Siku moja huo uzungu utamwonyesha mizungu" Kwa kuwa Mzee Busara hakupata usafiri wa haraka alimkuta mjukuu wake akichungulia mwanandani na baada ya saa chache alifunga safari kuenda kwa Baba kutungoja. Kisa hiki kilizungumziwa na kila mmoja

Siku moja Mzee Busara alipokuwa nyumbani akisikiliza redio alisikia tukio liliiomshtua sana. Mwajiriwa mmoja wa ndugu Mahewa alishikwa na dawa za kulevya katika uwanja wa ndege. Kumbe safari zote za ng'ambo zilikuwa za kalangua mihadarati



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

41. Jumba la ndugu Mahewa lilizungumziwa kotekote kwa kuwa
A. lilikuwa ikulu ya rais kabla ya kununuliwa na ndugu Mahewa
B. Lilikuwa limejengwa kwa mawe adimu
C. Kwa kuwa liliezekwa kwa vigae vyekundu
D. Katika eneo zima ndilo tu lililoanisi

42. Mwandishi anapiga chuku pale anaposema kuwa
A. Ndugu Mahewa alikuwa mmiliki wa jiji lote na watu wote
B. Ndugu Mahewa aliasi Molą baada ya kubarikiwa na mali
C. Usafiri wa ndugu Mahewa ulikuwa wa hewani
D. Ndugu Mahewa alikuwa na pesa nyingi

43. Aya ya tatu inamwonyesha Ndugu Mahewa kama mtu mwenye
A. Ukatili
B. Maringo
C. Ujinga
D. Ufidhuli

44. Mzee Busara alikuwa na bahati kumpata Ndugu Mahewa. Hata hivyo bahati yenyewe haikuwa na maana kwa kuwa.
A. Ndugu Mahewa alimkatiza mazungumzo kabla hata hajasema haja yake
B. Ndugu Mahewa alijifanya kuwa hakumtambua Mzee Busara
C. Mjukuu wake aliishia kuaga dunia licha ya juhudi zake
D. Ndugu Mahewa hakuvunja mipango yake ya kwenda ng'ambo siku hiyo

45. ..............."Nilikuwa katika kundi moja la tohara na babako" ...................... kwa nini Mzee Busara aliyasema maneno haya?
A. Ili Ndugu Mahewa amfahamu kwa wepesi na haraka
B. Kwa kuwa ulikuwa ukweli walipashwa tohara wakati mmoja na babake Ndugu Mahewa
C. Kwa kuwa kupashwa tohara kulimfanya mtu aheshimiwe sana
D. Alidhamiria kuulainisha moyo wa Nd gu Mahewa ili kupata mradi wake

46. Kwa nini Mzee Busara alimlaani Ndugu Mahewa kimoyomoyo?
A. Hakuelewa kwa nini hakuona umuhimu wa maisha ya mjukuu wake
B. Kwa kuwa alikosa kile alichotumainia
C. Kwa kuwa uzungu ungemwonyesha ndugu Mahewa Mizungu
D. Mzee Busara alijua wazi kuwa mwanawe alikuwa tayari ameaga dunia

47. Kuchungulia mwanandani ni
A. Kuaga dunia
B. Kuwa mahututi
C. Kuwa huongei
D. Kuwa na joto kali mwilini

48. Kulingana na makala haya, kifo cha mjukuu wake mzee Busara
A. kilisababishwa na ukosefu wa usafiri
B. kilisababishwa na hatua ya Ndugu Mahewa kwenda ng'ambo
C. kilisababishwa na utepetevu wa matabibu
D. kilisababishwa na ukosefu wa usafiri wa haraka

49. Mzee Busara alishangazwa na habari za redioni kwa kuwa
A. mfanyikazi alishikwa na maafisa wa polisi
B. hakuwahi kusikiliza habari kama hizo alizosikiliza
C. Hakudhani Ndugu Mahewa alikuwa mlanguzi wa mihadarati
D. Zilikuwa habari za kufisha moyo

50. Anwani mwafaka zaidi kwa makala haya ni
A Udhaniaye siye ndiye
B. Mungu hamsahau mja wake
C. Biashara haigombi
D. Mie nyumba ya udongo sihimili vishindo



Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com